## Mbarawa ataka kasi ujenzi wa uwanja wa ndege Dodoma ..Uk.2

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.18 Tanzania Bora ALHAMISI Februari 06, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




# Dkt. Samia aing'arisha Miaka 48 ya CCM Dodoma


>> Awaambia Wana CCM wajivunie mafanikio huku wakiendeleza mema

>> Asema CCM ina wanachama wengi zaidi ya Mil. 12 lakini wasibweteke

>> Atilia mkazo masomo wa ufundi ili vijana wajiajiri na kuajiri wenzao

HABARI UK.2





## Wassira: tumetesti Mitambo iko tayari

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mzee Steven Wassira jana alitimiza siku 17 tangu Mkutano Mkuu ulipomchangua kushika nafasi ya kuwa makamu mwenyekikti wa CCM Bara na tayari ameshafanya ziara katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita na Mara ambako kote amejiridhisha kuwa chama hicho kitashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.Makamu huyo mwenyekiti aliyasema

Inaendelea Uk. 2

## Dk. Mwinyi atoa neno kwa wana CCM

HABARI UK.2



# CCM FUNGA KAZI MIAKA 48 DODOMA

NA MWANDISHI WETU

SHEREHE za Chama cha Mapinduzi (CCM) kutimiza miaka 48 jana zililifunika kwa shangwe Jiji la Dodoma, kwa sherehe kubwa, ambapo mwenyekiti wake ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Akizungumza katika sherehe hizo, Dkt Samia alianza kwa kutoa rai kwa wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba huku akiwaondoa hofu dhidi ya wapinzani, lakini bila kuwadharau.

Rais Samia aliyasema hayo katika sherehe hizo ambazo ni rasmi kwa kuhitimisha kilele cha sherehe za CCM kutimiza miaka 48, zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ambapo pia alizishukuru Jumuia za chama hicho za UVCCM, UWT na Sekretarieti ya chama kwa hamasa pamoja na maandalizi ya mkutano huo.

Mwenyekiti huyo alikiri kuwa CCM ni chama imara na kina mtaji mkubwa wa wanachama ambao mpaka sasa wanafikia milioni 12 pamoja na wapenzi wengi, lakini alisisitiza kuwa hiyo isiwe sababu ya kubweteka kwa mafanikio hayo na badala yake wanatakiwa kupambana ili kuwatumikia Watanzania ili waione thamani ya chama kilichopewa ridhaa ya kuongoza serikali yao.

"Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri," alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Vilevile katika hotuba yake mwenyekiti huyo ametilia mkazo kuimarisha Jumuia ya Vijana UVCCM, ambao ameitaja kuwa ndiyo itakayojenga chama imara kwa kuandaa viongozi wajao watakaokiendeleza chama hicho na baadaye kushika hatamu za uongozi.

Kuhusu ajira kwa vijana, Dkt Samia alisema tayari wameanza kuboresha sekta ya elimu wezeshi ambayo inatoa fursa kwa vijana kusomea mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri pamoja na kuwaajiri wenzao, pia masuala ya utalii, uchumi wa bluu pamoja na elimu ni miongoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima Agosti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mzee Steven Wasira akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzania, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.

Vilevile sherehe kama hizo zimefanyika maeneo mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Ruvuma ambapo

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa huo, Oddo Mwisho alisema, uamuzi ya kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais wa Tanzania na Dkt Hussen Mwinyi kupeperusha bendera ya chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu ni sahihi kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya kwa Watanzania.



# WASSIRA:TUMETESTI MITAMBO IKO SAWA

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mzee Steven Wassira jana alitimiza siku 17 tangu Mkutano Mkuu ulipomchangua kushika nafasi ya kuwa makamu mwenyekikti wa CCM Bara na tayari ameshafanya ziara katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita na Mara ambako kote amejiridhisha kuwa chama hicho kitashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Makamu huyo mwenyekiti aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika mkutano wa kilele cha maamdhimisho ya kutimiza miaka 48, CCM zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema kuwa idadi kubwa ya Watanzania kwa dhati wanaonyesha imani yao kwa CCM na hasa Rais wake wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na utekelezaji wake wa ilan za CCM pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

"Kuna chombo Cha habari kilinipigi simu kikaniuliza kama tumeshaanza kampeni nikamwambia hapana ila tunatesti mitambo, napenda kusema kuwa sasa mitambo ipo tayari," alisema Mzee Wassira.

Alisema CCM inaongoza kwa ridhaa ya wananchi na Rais Dkt Samia ametekeleza ilani hivyo si rahisi kutokea kwa kuzuia 'mitano' tena kwake alisema.

# DKT. MWINYI ATOA NENO KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wana CCM kuhakikisha chama hicho kinaendelea kushika dola katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama inavyoelezwa katika Katiba ya CCM.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipohudhuria kilele cha maadhimisho ya miaka 48 ya CCM, yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma, aliwapongeza viongozi, wanachama, na wapenzi wa CCM kwa mafanikio makubwa yaliyojiri katika kipindi hicho cha miaka 48.

"Kwa hakika, wana-CCM tunayo kila sababu ya kufurahi na kujivunia mafanikio makubwa ambayo chama chetu kimeyapata. Sote tunawajibika kuyadumisha mafanikio haya kwa kuimarisha umoja na mshikamano. Tunakabiliwa na uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha chama chetu kinaendelea kushika dola," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, Dk. Mwinyi alisisitiza umuhimu wa kuwaandikisha wanachama wote katika daftari la wapiga kura na kuwahamasisha kwenda kupiga kura wakati wa uchaguzi, ili kuhakikisha CCM inashinda na kuendelea kushika dola.

"Watanzania wanaamini kauli ya muasisi wa Taifa letu, Hayati Baba wa Taifa [Julius Nyerere] aliposema; bila ya CCM imara nchi yetu itayumba, hivyo hatuna budi kuhakikisha kwamba chama chetu kinaendelea kuwa imara ili nchi yetu isiyumbe na izidi kupiga hatua za maendeleo," alisisitiza Dk. Hussein Mwinyi.

# Miaka 48 CCM dodoma haijapata kujtokea

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapainduzi CCM jana kiliandika historia kubwa kwa kufanya sherehe iliyofana kupita maelezo ya kuadhimisha miaka 48 tangu kilipoanzishwa mwaka 1977.

Sherehe hizo zilikuwa na kila aina ya shamrashamra huku Uwanja wa Jamhuri Dodoma lililokofanyika tukio hilo ukiwa umepambwa kwa ragi za Kijani na Njano zinazotumiwa na chama hicho

Licha ya sherehe hiyo kubwa chini ya Mgeni wake rasmi pia ikihudhuriwa na viongozi mbali mbali wa CCM na Serikali na Wastaafu pamoja na kutumbuizwa na wasanii mbalimbali ilionyesha kuvunja rekodi kwa ufanisi.

Jukwaa lilipambwa kwa rangi za kijani na njano, huku wanachama na mashabiki waliofurika wakionyesha mshikamano wao kupitia nyimbo na kauli mbiu za chama. Katika hotuba yake ya kipekee, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisimama imara mbele ya umati huo, akitoa mwito wa mshikamano kwa wanachama wote.

"CCM tuna wanachama zaidi ya milioni 12," alisema Dkt. Samia kwa sauti yenye kujiamini. "Tuna deni la kuhakikisha tunapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi ujao."

Kabla ya hotuba ya Dkt. Samia, CCM ilidhihirisha nguvu zake za kiuchumi kwa kuonyesha mabasi mapya, magari maalum kwa ajili ya wagombea urais Bara na Zanzibar, pikipiki, na baiskeli zitakazotumika wakati wa kampeni. Hili lilikuwa ni onyesho la ushindi wa kimkakati, linaloonyesha kuwa chama hicho si tu chama cha siasa bali pia chombo chenye mfumo imara wa kiutendaji.

Kwa upande wake, mgombea mwenza wa urais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, alionyesha utayari wake wa kushirikiana na Dkt. Samia, akiahidi kuimarisha kampeni kwa lengo la kuhakikisha CCM inazidi kung'ara.

"Nitahakikisha tunapata ushindi wa kishindo na kuimarisha nguvu za chama chetu," alisema Dkt. Nchimbi huku akishangiliwa na maelfu ya wanachama waliokuwepo.

Naye Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, alitumia fursa hiyo kusisitiza mafanikio makubwa ambayo CCM imeyapata, akiwakumbusha wanachama umuhimu wa kuyaendeleza mafanikio hayo.

"Chama chetu kimeonyesha uongozi thabiti na mafanikio makubwa kwa wananchi, na tuna kila sababu ya kujivunia," alisema Dkt. Mwinyi kwa kujiamini.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Steven Wassira, kwa upande wake, alitoa kauli ya uthibitisho kuwa hakuna chama kingine kinachoweza kushindana na CCM.

"Hakuna hati yoyote inayosema tulikubaliana na mtu yeyote kubaki madarakani. Ushindi wetu ni halali," alisema Wassira huku akiongeza msisimko kwa wanachama waliofurika uwanjani.

Sherehe hizi za kihistoria zimeacha hisia za matumaini makubwa kwa wanachama wa CCM, huku chama hicho kikijiandaa kuingia katika uchaguzi mkuu kwa kishindo na kuendelea kushika hatamu za uongozi nchini.



# MZEE WASSIRA AWAPA SOMO WANA CCM

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mzee Steven Wassira jana alitimiza siku 17 tangu Mkutano Mkuu ulipomchangua kushika nafasi ya kuwa makamu mwenyekikti wa CCM Bara na tayari ameshafanya ziara katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita na Mara ambako kote amejiridhisha kuwa chama hicho kitashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Makamu huyo mwenyekiti aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika mkutano wa kilele cha maamdhimisho ya kutimiza miaka 48, CCM zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema kuwa idadi kubwa ya Watanzania kwa dhati wanaonyesha imani yao kwa CCM na hasa Rais wake wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na utekelezaji wake wa ilan za CCM pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

"Kuna chombo Cha habari kilinipigi simu kikaniuliza kama tumeshaanza kampeni nikamwambia hapana ila tunatesti mitambo, napenda kusema kuwa sasa mitambo ipo tayari," alisema Mzee Wassira.

Alisema CCM inaongoza kwa ridhaa ya wananchi na Rais Dkt Samia ametekeleza ilani hivyo si rahisi kutokea kwa kuzuia 'mitano' tena kwake alisema.

Kabla ya mkutano wa jana Mzee Wassira alihudhuria Kongamano la Umoja wa wanawake wa CCM (UWT) na kuwaeleza jinsi chama hicho kilivyosimama kidete kuboresha sekta ya elimu.

Akizungumza wakati wa Kongamano hilo lilioandaliwa na Jumuiya ya Wanawake ya CCM (UWT) mjini Dodoma, Wasira alisema kuwa kabla ya Uhuru, wanawake walikumbwa na changamoto kubwa ya kutokuwa na fursa za kupata elimu bora kama ilivyokuwa kwa wanaume.

"Katika kipindi cha kabla ya uhuru, wanawake wa Tanzania walikosa haki ya kupata elimu sawa na wanaume, na walikosa nafasi katika maeneo mengi ya kijamii na kiuchumi," alisema Wasira. "Lakini kupitia uongozi wa CCM, tumefanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu, na leo hii wanawake wengi wameweza kupata elimu bora, jambo ambalo limewafungua milango ya fursa nyingi za kiuchumi na kijamii."

Makamu Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa juhudi za CCM za kuhakikisha elimu bora kwa wanawake zimesaidia kupunguza pengo la kijinsia katika sekta ya elimu, na hivyo kuleta usawa katika jamii.

# SAMIA, MWINYI WAMLILIA AGAKHAN

NA DOTTO KWILASA,

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi wametuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Kiongozi wa kiroho wa madhehebu ya Ismailia duniani na mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan.

Rais Samia amesema amepokea kwa huzuni taarifa ya kifo cha Mwanamfalme Karim Al-Husseini, Aga Khan IV.

"Kwa niaba ya Serikali na Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutoa rambirambi zetu za dhati na za moyoni kwa familia ya Mwanamfalme Karim, Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan, na Jumuia ya Waislamu wa Ismailia," amesema.

Rais Samia amesema Tanzania inaungana na jumuiya hiyo kuomboleza kifo cha kiongozi huyo mashuhuri na mwenye maono, ambaye kazi yake imegusa na kubadilisha maisha ya mamilioni ya watu kote ulimwenguni na kwamba fikra na maombi ya Watanzania yako nao katika kipindi hiki kigumu.

Kwa upande wake Rais Mwinyi amesema kwa niaba ya Serikali na Watu wa Zanzibar, anatoa pole kwa familia ya kiongozi huyo, Jumuia ya Waismailia, na wote walioguswa na alama aliyoacha.

"Tunapoomboleza msiba huu mkubwa, pia tunasherehekea kiongozi ambaye mazuri aliyofanya katika maisha yake yataendelea kuhamasisha vizazi vijavyo," amesema Rais Mwinyi.

Aga Khan amefariki dunia huko Lisbon, Ureno akiwa na umri wa miaka 88.

KIONGOZI Mkuu wa 49 wa Madhehebu ya Shia Ismailia na mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), Mtukufu Aga Khan, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 88 jijini Lisbon, Ureno, Februari 4, 2025.

Mtukufu Aga Khan, anayefahamika kama Karim Al-Hussaini Aga Khan IV, alijulikana kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha ustawi wa binadamu kupitia miradi mbalimbali duniani.

"Katika maisha yake, Aga Khan IV alisisitiza Uislamu ni imani inayohimiza kujitolea, uvumilivu, na utu wa mwanadamu," inasema taarifa rasmi kutoka Ureno.

Alizaliwa Desemba 13, 1936, Geneva, Uswisi, na alikulia Nairobi, Kenya. Alipata elimu katika shule ya Le Rosey nchini Uswisi na Chuo Kikuu cha Harvard, Marekani, ambako alisomea masomo ya Uislamu.

Baada ya kifo cha baba yake, aliacha ndoto zake za soka na masomo ya uzamivu ili kuchukua wadhifa wa Imamu wa 49 wa madhehebu ya Shia Ismailia.

Mbali na uongozi wa kidini, alihimiza maendeleo ya jamii kupitia sekta za afya, elimu, habari, utamaduni, na ustawi wa jamii.

Alianzisha miradi kama Shule na Chuo Kikuu cha Aga Khan, Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi wa Aga Khan (AKFED), na Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), ambao umeleta maendeleo katika afya, elimu, na uchumi, hasa Afrika Mashariki.

Nchini Tanzania, mchango wake unaonekana kupitia Mwananchi Communications Limited (MCL) na Hospitali za Aga Khan, huku nchini Kenya alianzisha Nation Media Group (NMG) na viwanda kadhaa.

AKDN imeleta mafanikio katika jamii barani Afrika, Asia, na Mashariki ya Kati kwa kusaidia maendeleo katika maeneo yaliyoachwa nyuma.

Uteuzi wa Imam wa 50 na mazishi Imam wa 50 wa urithi tayari ameteuliwa, na atatangazwa rasmi baada ya wasia wa Mtukufu Aga Khan IV kusomwa katika siku zijazo. Taratibu za mazishi zitatangazwa hivi karibuni.

Kifo cha Mtukufu Prince Karim Aga Khan IV kinahitimisha enzi ya uongozi wa kipekee na huduma kwa binadamu, lakini urithi wake wa maendeleo na ustawi wa kijamii unaendelea kuhamasisha vizazi vijavyo.

&&&

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga ametoa rai kwa wananchi kuunganisha huduma ya umeme wakati miradi mbalimbali ya umeme inapotekelezwa ili kuepuka gharama inayoweza kutokea pale miradi inapokuwa imekamilika.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Februari 05 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Tanga Mjini Mhe. Ummy Mwalimu aliyetaka kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kuwaunganishia umeme wa gharama nafuu kwa Wananchi wa maeneo ya Pembezoni yenye sifa za Vijiji mkoani Tanga.

"Katika kurahisisha upatikanaji wa huduma ya umeme wa bei nafuu kwa maeneo ya pembezoni mwa Jimbo la Tanga Mjini, Serikali kupitia REA inaendelea kutekeleza Mradi wa Peri-Urban III", Amesema Mhe. Kapinga.

Ameongeza kuwa mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi OK Electrical kwa kuunganisha wateja kwa baadhi ya mitaa kwa gharama ya shilingi 27,000 ambapo mpaka sasa jumla ya wateja 1,302 wameshaunganishiwa huduma ya umeme. Mhe. Kapinga amesema maeneo ya Tanga Mjini yaliyosalia yapo kwenye mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 vya kila Mbunge (HEP IIA) ambapo Jimbo la Tanga Mjini litapelekewa umeme kwenye mitaa 15.

Akielezea kuhusu Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwaunganishia umeme wananchi kwa mkopo, Mhe. Kapinga amesema Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya umeme ili kuwafikia wananchi kwa gharama nafuu ya shilingi 27,000/-.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa TANESCO ilishawahi kuwaunganishia wananchi kwa kuwakopesha ambapo ilikutana na changamoto ya wananchi kutokuwa na utayari ya kulipa madeni yao.

Akijibu swali Mbunge wa Ilemela, Mhe. Angelina Mabula aliyetaka kufahamu mitaa ya Masenene, Kilabela, Bujingwa, Nyanguku, Butimba na Toronto itapatiwa umeme kutokana na kuondolewa katika mitaa 15 inayotekelezwa na REA kutokana na kuwepo kwa njia kubwa ya umeme.

Akijibu swali hilo Mhe. Kapinga amesema miradi ya vitongoji ni ya ujazilizi ambayo inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo ambayo yamepitiwa na njia kubwa ya umeme ambapo pamoja na mitaa hiyo itanufaika.





# TAA ZA BARABARANI DAR KUPATA SULUHU YAKE

NA MWANDISHI WETU

TAFAKURI Angavu leo inaangazia changamoto ya taa za kuongozea magari (taa za trafiki), ambazo ni muhimu kwa kudhibiti mtiririko wa magari na kuhakikisha usalama barabarani jijini Dar es Salaam. Pamoja na umuhimu wake, mara kwa mara taa hizi zimekuwa zikipata hitilafu, hali inayosababisha msongamano na wakati mwingine ajali, na usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

Sababu za Tatizo

Uchunguzi wa safu hii ya Tafakuri Angavu imebainisha sababu kadhaa zinazochangia kuzimika kwa taa hizi na baadhi ya hizo ni: Mosi, ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara. Taa za trafiki zinahitaji mpango endelevu wa matengenezo ambao mara nyingi hukosekana.

Pili ni changamoto ya umeme. Mfumo wa umeme usio wa uhakika wakati mwingine unasababisha taa hizi kushindwa kufanya kazi ipasavyo.

Tatu, uharibifu wa miundombinu: Ajali za barabarani, wizi wa vifaa, na mazingira duni ya barabara vinaathiri ufanisi wa taa za trafiki. Nne, ukosefu wa usimamizi thabiti. Ufuatiliaji wa hali ya taa hizi mara nyingi hufanyika pale kunapokuwa na malalamiko ya wananchi.

Athari zinazotokana na tatizo

Taa zisipofanya kazi husababisha changamoto kadhaa kubwa ikiwa ni msongamano wa magari kwani kukosekana kwa mwongozo wa taa mambo huwa shaghalabaghala na kuleta usumbufu mkubwa.

Lakini pili, ajali za barabarani huweza kutokea hasa katika maeneo yenye magari mengi kama Mwenge, Magomeni, Morocco na kadhalika.

Suluhisho

Ukijua sababu ya tatizo ni rahisi kutafuta suluhisho, hivyo Tafakuri Angavu inapendekeza hatua hizi kuchukuliwa.

Mosi, ni kufunga taa za trafiki zinazotumia nishati jadidifu kama jua ili kupunguza utegemezi wa umeme wa gridi. Pili, kuwepo na mpango endelevu wa matengenezo. Mamlaka husika zinapaswa kuhakikisha taa hizi zinahudumiwa mara kwa mara.

Tatu, kuimarisha ulinzi wa miundombinu ikiwa na kufunga camera za ulinzi. Kudhibiti wizi na uharibifu wa makusudi. Na nne, elimu kwa wananchi inatakiwa kwa maana ya kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kulinda miundombinu hii na kutoa taarifa za changamoto mapema.

Unaweza kukuta vyombo vya habari kama redio na televisheni vimeandaa vipindi vya usalama barabarani lakini ni nadra kusikia elimu ya umuhimu wa ulinzi na utunzaji wa miundombinu hii ikitolewa.

Hitimisho

Kuzimika kwa taa za kuongozea magari jijini Dar es Salaam ni changamoto kubwa inayohitaji kushughulikiwa. Kupitia Maendeleo ya teknolojia, matengenezo endelevu, na ushirikiano wa jamii, tatizo hili linaweza kupatiwa suluhisho la kudumu.

# MBARAWA ATAKA KASI UJENZI WA UWANJA WA NDEGE DODOMA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Uchukuzi Prof Makame Mbarawa amehimiza wasimamizi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Msalato ambao ni TANROADS na TAA kuhakikisha Mkandarasi anaongeza kasi zaidi ya umaliziaji wa hatua zilizobaki ili kukabiliana na mvua zinazotarajiwa kuanza kunyesha

Mbarawa ameyasema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege kilichopo Msalato Jijini Dodoma iliyofanyika Tarehe 30 Januari,2025.

"Ninapongeza kwa dhati hatua zilizofikiwa, nimeona sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa uwanja wa kurukia na kutua ndege unaogharimu shilingi Bil 165.65 kazi inaendelea vizuri na imefikia asilimia 84 natoa rai msimamieni Mkandarasi aongeze kasi hapa ili mvua zinazotarajiwa kuanza mwezi Machi mwaka huu zisimkwamishe" amesisitiza Mbarawa.

Amesema Mkandarasi asimamiwe vyema afanye kadri awezavyo na kwa thamani halisi ya fedha uwekaji wa rami umalizike ndani ya wiki mbili sababu mwezi wa tatu kutakuwa na mvua nyingi na huwezi kuweka rami wakati wa mvua.

Aidha ameongeza kuwa kazi zitakazobaki za kufunga mifumo ya kuongozea ndege sambamba na sehemu ya pili ya ujenzi wa jengo la abiria ambao umefikia asilimia 70 ambavyo vinaweza kufanywa taratibu hata kipindi cha mvua vitakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2025 na uwanja utakuwa tayari kwa matumizi ambapo utaleta tija kwa Nchi na wakazi wa Dodoma na mikoa ya jirani.

Akitoa taarifa za mradi Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Dodoma Mha Zuhura Amani amesema mpaka sasa utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri ambapo ujenzi wa uwanja umefikia asilimia 84, na upande wa majengo yote unaohusisha jengo la kushukia na kupandia abiria na jengo la kuongozea ndege vimefikia asilia 51 kwa ujumla na wataongeza kasi ya usimamiaji ili vikamilike kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha ili wananchi waanze kukivunia maendeleo yanayoletwa na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhi Hassan.

# Tanzania yapaa sekta ya fedha




NA MWANDISHI WETU

TANZANIA imepiga hatua kubwa kwenye sekta ya fedha kwa mujibu wa ripoti ya Absa ya viashiria vya Masoko ya Fedha - AFMI ( Absa Financial Markets Index ) 2024 iliyozinduliwa leo Jijini Dar es Salaam, ikipanda kutoka alama 50 hadi alama 52, na kujikita katika nafasi ya 12 miongoni mwa mataifa 29 yaliyotathminiwa barani Afrika.

Ikiwa katika mwaka wake wa nane, AFMI ni ripoti maarufu barani Afrika, ambayo hupima maendeleo ya sekta ya fedha katika nchi za Afrika, ikitathmini vigezo sita vikuu, ambavyo ni kuenea kwa soko, upatikanaji wa fedha za kigeni, uwazi kwenye soko na kanuni, maendeleo ya mifuko ya penseni, mazingira ya uchumi ngazi ya kitaifa, na kutekelezeka kwa makubaliano ya kifedha.

Akiongea katika hafla ya uzinduzi wa ripoti ya AFMI , Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, ambaye alikuwa ni mgeni rasmi, alipongeza kundi la makampuni la Absa Group kwa kujitolea kukuza uwazi na ufanisi katika masoko ya fedha barani Africa kupitia ripoti ya AFMI. " Mafanikio yaliyobainishwa katika ripoti hii ni ushahidi wa juhudi za ushirika miongoni mwa serikali, Benki Kuu ya Tanzania, na washirika wa soko la fedha katika kuboresha masoko hayo," alisema.

> *Pamoja na kuwa kuna maendeleo yamepatikana, bado kuna kazi ya kufanya hasa kwenye maeneo kama mifuko ya pensheni na mifumo wa kisheria,"*

Moja ya maeneo ambayo Tanzania imeonyesha kupiga hatua ni Upatikanaji wa Fedha za Kigeni, ikipanda kutoka alama 53 hadi alama 60, hasa kutokana na Benki Kuu ya Tanzania kuchapisha Miiko ya utendaji katika Soko la Fedha za Kigeni Miongoni mwa Mabenki ( Interbank Foreign Exchange Market code of conduct,), ikiingiza kanuni 52 kati ya 55 zinazotambuliwa kimataifa ( FX Global Code Principles).

Eneo la pili ni Uwazi katika Mazingira ya uchumi ngazi ya Kitaifa, ambapo imepanda kutoka alama 80 hadi 85, ikichagizwa na uwazi, ikiwemo umma kuruhusiwa kufahamu ratiba ya mkutano wa sera ya fedha, mfumuko mdogo wa bei, na kupungua kwa uwiano wa mikopo chefuchefu kwenye makampuni ya biashara.

Eneo la tatu ni uwezo wa soko la fedha kufikia watu wengi zaidi, ambapo maendeleoa katika nyanja hii yanatokana na kutolewa kwa dhamana ya makampuni (corporate bonds) zenye thamani ya Dola za Marekani 300m, na kuziduliwa kwa huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo zinazorandana na maadili ya Dini ya Kiislamu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Obedi Laiser, alisisitiza umuhimu wa ripoti ya AFMI katika kuchochea kukua kwa masoko ya fedha barani Afrika. " Kupanua masoko ya fedha na vilevile kuyafanya yafikie watu wengi zaidi ni muhimu kwa hatua inayofuata ya maendeleo barani Afrika," alisema mkurugenzi huyo. " Tunayo fahari kushirikiana na OMFIF katika kutayarisha ripoti hii, ambayo inafanya kazi kama dira miongoni mwa watunga sera na wawekezaji.

Tukio la uzinduzi wa ripoti ripoti hiyo inayoheshimika ilihudhuriwa na wadau, watunga sera, na watalaam wa masuala fedha, ambapo walipata fursa ya kubadilishana mawazo huku wakitathmini taarifa hiyo na jinsi gani inahusiana na utendaji wa masoko ya fedha nchini Tanzania.

Uzinduzi huo vilevile ulihudhuriwa na maofisa wakuu wa Absa Group, ambao walichangia uzoefu wao kwenye maendeleo yanayojitokeza kwenye sekta ya fedha ambayo yanaamua muundo wa masoko ya fedha Afrika, ikiwemo teknolojia za kidijitali, na juhudi za kuboresha vyombo vya sheria na vinavyosimamia kanuni.

Ripoti hiyo, inayotayarishwa kwa kushirikiana na OMFIF, inatoa taarifa muhimu kwa wawekezaji wa watunga sera, huku ibainisha fursa kwa upande moja, na vilevile maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho kwenye masoko ya fedha barani Afrika.

Wajkati huohuo, ripoti hiyo imebanisha maneo mawili ambayo Tanzania inapaswa kuyafanyia maboresho, ikiwemo mifuko ya pensheni, ambapo ripoti imedokeza haja ya kuimarishwa kwa uwezo wa kuwekeza wa wadau wa ndani. Na vilevile uboreshaji wa mfumo wa sheria ili kuinua kiwango cha imani ya miongoni wawekezaji.

Richard Magongo, Mkurugenzi wa Bodi - Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Mazingira Hatarishi, kwa niaba ya Paul Makanza, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Benki ya Absa Tanzania, pamoja na kuwashukuru waliohudhuria hafla hiyo, alisisitiza haja ya kufanyia maboresho ya maeneo nchini Tanzania yalioainishwa kwenye ripoti.

" Pamoja na kuwa kuna maendeleo yamepatikana, bado kuna kazi ya kufanya hasa kwenye maeneo kama mifuko ya pensheni na mifumo wa kisheria," alisema Magongo. " Absa inaahidi kuwa itaendelea kushirikiana na wadau wote kuhakikisha masoko ya fedha nchini Tanzania yanaendelea kukua."

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


### BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

### MAWASILIANO

JAMVI MEDIA GROUP





*Sehemu ya watumishi wa Wakala wa Vipimo wakiwa kazini Kituo cha Misugusugu Mkoa wa Pwani.*

## UCHAMBUZI

# Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# UNDP YAJA NA WIKI YA UBUNIFU

NA MWANDISHI WETU




WAKATI Dunia ikienda kasi katika teknolojia Tanzania itanufaika na ushikiano wa Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania kupitia programu yake ya FUNGUO, Vodacom Tanzania, na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) ambapo ushirikiano huo umefanikisha kuandaa Wiki ya Ubunifu Tanzania 2025 (IWTz2025). Anaripoti Mwandishi Wetu, Dar es Salaam … (endelea).

ushirikiano huu utazidi kuimaisha Tanzania kwenye maendeleo ya Teknolojia na ubunifu. Wiki hiyo itakayoanza tarehe 12 Mei mpaka tarehe 16 Mei 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Wakati huo huo kutafanyika mkutano wa Future Ready wa Vodacom.

Kauli mbiu ya mkutano huo itakuwa “Ubunifu kwa Maendeleo Jumuishi na yenye Ustahimilivu”, ikilenga kuonyesha dhamira ya pamoja yakujenga jamii endelevu, jumuishi na ya kisasa katika kutatuachangamoto ya ajira kwa vijana kwenye zama hizi za kidijitalina kuchochea ukuaji wa kibiashara kupitia tafiti na ubunifu.

Leo tarehe 5 Februali 2025 Taasisi hizo zimetangaza ushikiano huo mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Phillip Besiimire amesema ushirikiano huo utaleta mabadiliko katika sekta ya ubunifu nchini Tanzania, kwa kuunganisha wabunifu na wajasiriamali wa kimataifa kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

“Tunalenga kuleta mitazamo na taaluma za kimataifa kwenye mijadalahii na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha mabadiliko yakidijitali, sambamba na kuanzisha mifumo ya ikolojia yaubunifu inayoongozwa na vijana.

“Jitihada za Vodacom za kutumia teknolojia kwa lengo la kuboresha maisha ndiozinazounda msingi wa ushirikiano huu unaoendeshwa na maonoyanayofanana ya kuwawezesha watanzania kuendelea kupitiaUchumi wa kidijitali ulioendelevu na jumuishi.”

Aidha amesema kuwa mkutano wa Vodacom wa Future Ready Summit (FRS2025) ni tukio linaloweka msingi wa maadhimisho hayo pamoja nakuibeba kauli mbiu ya “Kubadilisha hatma ya miji: Usasa, Uendelevu na Jumuishi”, ambayo inazungumzia umuhimu wa kuibadili miji ya Tanzania kwa ajili ya kutatua changamoto zinazotokana ukuaji wa kasi, mabadiliko ya tabia nchi namabadiliko ya teknolojia.

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa UNDP Tanzania, Shigeki Komatsubara, amesisitiza dhamira ya UNDP ya kujenga mfumo wa ubunifuulio jumuishi na wenye ustahimilivu.

“Tunatambua kuwa ubunifu ni nyenzo muhimu katika kushughulikia changamoto za maendeleo endelevu na kuunda fursa shirikishi. Kupitiaushirikiano huu, tunalenga kuwainua Watanzania, hasa vijana nawanawake, kuwa chachu ya mabadiliko chanya.

“Wiki ya Ubunifu Tanzania 2025 (IWTz2025) itaonyesha ari ya ubunifuTanzania kwenye jukwaa la kimataifa, kuvutia uhamasishaji naushirikiano kupitia na mifumo iliyofanikiwa duniani.”

Kuhusu ajenda zitakazohusika katika maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu ni hayo itahusisha mijadala mtambuka, warsha na maonyesho, huku lengo likiwa ni Mustakabali wa miji mahiri, endelevu na jumuishi, Uwezeshaji wa vijana kwenye zama za kidijitali, Uboreshaji wa tafiti na ubunifu kwa ajili ya biashara

Akizungumza kwa niaba ya Serikali, Mkurugenzi wa Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk Athumani Ngumia alisema mchango muhimu wa ushirikiano huo ni kukuza ubunifu.

“COSTECH imejidhatiti kuwaunganisha wadau kwa lengo la kuchochea utafiti, teknolojia na ubunifu ambao unaendana navipaumbele vya nchi katika maendeleo na maono ya mwaka2050. Maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu kwa mwaka 2025 nijukwaa pekee kwa ajili ya sekta binafsi na umma kupeleleza nakutekeleza masuluhisho kwa ajili ya ukuaji endelevu.”

Wiki ya ubunifu 2025 (IWTZ2025) na mkutano wa Future Ready Summit (FRS2025) inatarajia kuwaleta pamoja washiriki, wazungumzaji na wabunifu kutoka Tanzania, Afrika na sehemu mbalimbali duniani na kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana maarifa, kuendeleza ushirikiano wenye tija na kuhamasishamawazo yenye kuleta mabadiliko.

Washiriki wa matukio haya wanahamasishwa kutekeleza shughuli mbalimbali sambamba na matukio hayo muhimu kwa lengo la kuhakikisha watu wengi zaidi nchini wanawezakunufaika na mikutano hiyo itakayo kuwa inafanyika kwenyeKituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere.

Wakati huo huo Meneja Program kutoka FUNGUO Joseph Manirakiza ametumia nafasi hiyo kuelezea kwa kina umuhimu wa ushirikiano huo sambamba na kutambua mchango wa bunifu katika kukuza maendeleo endelevu

Kuhusu Programu ya FUNGUO ni kwamba inajitolea kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) nchini Tanzania kwa kutumia mbinu shirikishi inayolenga kusaidia maendeleo ya biashara bunifu na zinazozingatia athari chanya kwa jamii, hususan kwakuimarisha mazingira ya ubunifu kwa wajasiriamali na biasharandogo na za kati (MSMEs).

Aidha FUNGUO inatambua kuwa kusaidiana kukuza biashara hizo siyo tu kutachangia kuongeza ajira, hususan kwa wanawake na vijana, bali pia kutaboresha kipato, kuboresha hali ya maisha, na kuchochea maendeleo jumuishi naendelevu.

Pia Mpango huo unafadhiliwa kwa pamoja na Umoja wa Ulaya(kupitia Mpango wa BEGIN), Serikali ya Uingereza (kupitiaMpango wa Ushirikiano wa Teknolojia na Ubunifu barani Afrika – ATIP), na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa(UNDP).

FUNGUO unatekelezwa na UNDP Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja waMataifa (UNCDF). Ushirikiano huu wa wadau mbalimbali unahakikisha ufanisi na athari chanya katika mazingira yaubunifu nchini Tanzania.

Kwa kushirikiana kwa karibu na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) pamoja nataasisi nyingine za serikali, FUNGUO inalenga kuchangia maendeleo endelevu nchini kwa kuweka mazingira wezeshi kwabiashara bunifu na MSMEs.

Kuhusu Vodacom Tanzania ni mtoa huduma wa mawasiliano anaeongoza nchini Tanzania, ikiwa na mtandao wa data wa kasi zaidi. Tunahudumia zaidi ya wateja milioni 26.3. Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu ni sehemu ya Vodacom Group yenye usajili nchini Afrika Kusini, ambayo nayo inamilikiwa naVodacom Group Plc yenye makao makuu Uingereza.

Wakati COSTECH ni Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 1986.Pia ni shirika la umma linalohusika na kuratibu na kukuza shughuli za utafiti na maendeleo yateknolojia nchini.

Pia, inatoa ushauri kwa serikali kuhusumasuala yote yanayohusiana na sayansi, teknolojia, na ubunifu(STI) kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamiinchini Tanzania.COSTECH inafanya kazi chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

*Matukio mbalimbali kwenye uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma yakionyesha wana CCM wakisherehekea miaka 48 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi yanayofanyika mkoani humo kitaifa, jana. Katika sherehe hiyo Viongozi, wanasiasa na wasanii pamoja na watu maarufu wamehudhuria katika maadhimisho hayo.*









*Matukio mbalimbali kwenye uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma yakionyesha wana CCM wakisherehekea miaka 48 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi yanayofanyika mkoani humo kitaifa, jana. Katika sherehe hiyo Viongozi, wanasiasa na wasanii pamoja na watu maarufu wamehudhuria katika maadhimisho hayo.*

# MAFAO KWA WASTAAFU YAPATIWE SULUHU YA KUDUMU




NA MWANDISHI WETU

KWA muda mrefu kumekuwa na kilio kuhusu kucheleweshwa kwa malipo ya wastaafu kwa sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni kutokuwapo kwa taarifa zao Hazina au kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ambazo zinapaswa kuwasilishwa na waajiri kabla ya mfanyakazi kufikia ukomo wa ajira yake.

Mifuko hiyo, ambayo hulipa mafao ya watumishi wa umma na wale wa sekta binafsi pamoja na Hazina ambako hulipwa mafao ya wastaafu kama vile kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, pia imekuwa ikichelewesha malipo hayo ama kwa sababu waajiri hushindwa kuwasilisha makato ya kila mwezi ya wafanyakazi au kushindwa kupeleka taarifa za wafanyakazi ili uandaaji malipo kabla ya kustaafu ufanyike.

Kutokana na kuwapo kwa changamoto hiyo, baadhi ya watumishi wamekuwa wakihangaika kufuatilia mafao yao na wakati mwingine kukata tamaa na hata kufariki dunia kabla ya kuyafaidi licha ya kutumia nguvu zao nyingi katika kufanya kazi. Pia hali hiyo imewafanya baadhi ya watumishi walioko bado kwenye ajira kuona kama vile kustaafu ni adhabu.

> *Waajiri wote, zikiwamo taasisi za serikali, wanapaswa kupeleka taarifa za wafanyakazi ambao wamebakiza muda mfupi kustaafu ili waandaliwe mafao yao na hatimaye kuyapata baada ya kuondoka katika utumishi.*

Mfano wa watu ambao wamefanya kazi na kuanza kuhangaika kufuatilia mafao ni askari wastaafu wa Jeshi la Polisi ambao juzi wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu Bungeni, mbunge mmoja alihoji ni kiasi gani ambacho wastaafu hao wa chombo kilichopewa dhamana ya kusimamia usalama wa raia na mali zao.

Katika majibu ya serikali ilielezwa kuwa wastaafu hao wanadai mafao ya zaidi ya Sh. bilioni 97.1 na kwamba kati ya hizo, Sh. bilioni 75.2 zmepelekwa Hazina kwa ajili ya malipo baada ya kufanyika kwa uhakiki wa wastaafu hao. Pia serikali ilisema mafao ya takribani Sh. bilioni 21.9 bado yanahakikiwa kabla ya watumishi hao kulipwa.

Tatizo kubwa, kwa mtazamo yakinifu, linaloonekana hapa ni uhakikiwa wa wastaafu hao baada ya kumaliza utumishi wao wa jambo ambalo lilipaswa kufanyika miezi au hata mwaka kabla ya kufikia muda wa kuondoka kwenye ajira. Badala ya kufanya hivyo, kazi hiyo ya uhakiki imekuwa ikifanyika baada ya mtu kutoka katika utumishi jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wahusika.

Chanzo kikubwa cha kuwapo kwa changamoto hiyo ni majina na taarifa za wahusika kutokuwa katika mfumo na matokeo yake mtu anaanza kuhakikiwa upya baada ya kustaafu. Inakuwaje mtu aanze kuhakikiwa baada ya kustaafu wa kuulizwa mwaka aliozaliwa, lini alipandishwa cheo na kama anadaiwa na taasisi yoyote ya fedha iwapo aliwahi kukopa na hajamaliza deni kabla ya kustaafu.

Kuwapo kwa hali hiyo pia hutengeneza mazingira ya rushwa kwa baadhi ya watumishi wa Hazina na mifuko kutaka wastaafu hao kutoa chochote ili wasizungushwe na milolongo ya kufuatilia mafao. Kwa kuepuka usumbufu huo, baadhi ya wahusika wamekuwa wakaingia katika mtego huo kwa sababu ya kukataa kuchoshwa na hadithi ya 'njoo kesho, njoo kesho'.

Suala la mafao kwa wastaafu kwa sasa limekuwa sawa na hadithi isiyokuwa na mwisho. Ni vyema sasa serikali ikachukua hatua madhubuti ili kukomesha suala hili na kurejesha furaha kwa wastaafu ambao kwa sasa wanaona kufikia hatua hiyo ni kama mwisho wa maisha yao.

Waajiri wote, zikiwamo taasisi za serikali, wanapaswa kupeleka taarifa za wafanyakazi ambao wamebakiza muda mfupi kustaafu ili waandaliwe mafao yao na hatimaye kuyapata baada ya kuondoka katika utumishi.

Pia, kama kuna uwezekano, sheria inayohusu mifuko ya jamii, pensheni na mafao kwa wastaafu ifanyiwe marekebisho ikiwamo kuweka kipengele cha adhabu kwa mwajiri ambaye atachelewesha kupeleka taarifa za mtumishi kabla ya kustaafu.

# Unaikumbuka Marijani na Vick?

NA MWANDISHI WETU

WAKATI ikikaribia kumbukuzi la kifoi cha mwanamuziki mahiri aliyewahi kuokea katika ardhi ya bTanzania Marijan Rajab, leo tukumbuke moja ya nyimbo zlizotunga enzi ya uhai wake.

Marijani alianza kutamba katika tasnia ya muziki akiwa na bendi ya STC mwaka 1970 hadi 71, kisha akahamia katika bendi ya Safari Trippers mwaka 1972 na kurekodi albam ya kwanza tarehe 19.1.1972, yenye nyimbo kama Rosa nenda Shule, Mkuki Moyoni, Rafiki si mtu mwema na nyingine kadha.

"VICK ee ungenijulisha mapema, mawazo kama yamebadilika ili niweze kumtafuta mwingine awezaye kulisakata "Bomboka", usinikondeshe buree mwana wa mwenzio, wakati wewe mwenyewe hata hunijali, hebu nijulishe Vick ee ili nijue moja"...

Haya ni maneno yaliyomo katika wimbo wa "Vick" uliotungwa na Marijan Rajab muda mfupi aliporejeshwa katika bendi ya Dar international na kupewa jukumu la kuiongoza bendi hiyo mwaka 1979.

Muda mfupi ulipotekodiea wimbo huo, mashairi yake yaliimbwa kila Kona na mashabiki kila rika wazee kwa Vijana, wake kwa wauume.

Licha ya kubamba hivyo, lakini kwa Marijani ulikuwa ni wimbo uliompa presha sana kutokana na usumbufu alioupata kutoka kwa wapigaji wa gitaa la solo.

TUJIKUMBUSHE

Awali Marijani alikuwa ni mwanzilishi wa bendi ya Dar international mwaka 1977 baada ya bendi ya Safari Trippers aliyoitumikia muda mrefu kuvunjika, kiongozi na mwenye sauti katika bendi hiyo mpya alikuwa ni Abel Baltazal huyu alikuwa pia ni rafiki wa mmiliki Zacharia Ndebameye, aliyewahi kusoma nae huko Mjesani Tanga.

Baada ya kurekodi albam ya Rufaa ya kifo Mwezi Machi 1978 likaanza bifu kati ya Marijan na Abel, kisa na mkasa Abel alichukizwa na uimbaji wa Marijani, akidai unafanana na ule wa Safari trippers.

Abel alitaka bendi ya Dar international isipige muziki unaofanana na bendi yoyote ile bali itengeneze aina yake ya muziki.



Abel akadiriki kumtimua Marijan alipomkataza kuendelea na mazoezi ya wimbo Kidudu mtu ambao yeye aliupinga kwa madai unafanana na Safari Trippers.

Lakini Kama zali kwa Marijani, hatimaye Abel na wanamuziki kadha wakapata "dili" la kwenda kuanzisha bendi ya Orchestra Mlimani Park.

Uongozi wa Dar international bila kupinda kushoto wala kulia, wakakubaliana kuwa ni Marijan pekee ndiye anayeweza kuiokoa bendi hiyo.

Hivyo wakaamua kwenda kumpigia nagoti nyumbani kwake mtaa wa "Somali na Living stone" na kufanya kikao kilichokuwa na mafanikio katika hotel ye "Keys" iliyopo jirani na nyumbani kwake.

Marijan haraka sana akaunda upya kikosi chake, lakini katika upigaji la solo moyo wake wote alimwamini Patrick Kamaley na kiasi Christopher Kasongo.

Mkakati wa Marijani kwanza ni kuhakikisha anatunga nyimbo zinazotaja majina ya mashabiki wake wa eneo la Kariakoo, hii ikasababisha bendi hiyo ianze na mtaji wa mashabiki kutoka Kariakoo.

Baada ya mazoezi makali ya nyimbo kama Mayasa, Zuwena, Vick nk bendi ilitaka kwenda kurekodi katika studio za RTD.

Hapo ndipo ilipotokea "Songombingo" kwani mpiga solo huyo namba moja akatoweka ghafla, akatafutwa kila kona asipatikane.

Kumbe mwamba Kamaley, aliibukia Tanga na kijiunga na Tanga international.

Kasongo naye akarekodi nyimbo kadha ulipofika wimbo wa Vick naye akaingia mitini.

Afadhali Mpiga "Saxafoni" Mafumu bilali naye kumbe alikuwa mkali pia katika upigaji gitaa, ndipo akaokoa jahazi na kurekodi wimbo huo, ambao nao ulibamba vya kutosha.

Kutokea hapo Dar international ikaendelea kubadilisha wapiga gitaa la solo kadha wa kadha hadi ilipozimika rasmi mwaka 1986.

# Dkt. Samia aja na mkakati kuondoa ukosefu wa ajira kwa vijana



NA MWANDISHI WETU

MWENYEKITI WA Chama Cha Mapinduzi Dkt Samia Suluhu Hassan, ametoa rai kwa wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba huku wakiondoa hofu dhidi ya wapinzani, lakini bila kuwadharau.

Aliyasema hayo alipokuwa akihutunbia katika kilele cha sherehe za CCM kutimiza miaka 48, zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma ambapo pia alizishukuru Jumuia za Chama hicho UVCCM, UWT na Sekretarieti ya chama hicho kwa hamasa pamoja na maandalizi ya mkutano huo.

Mwenyekiti huyo alikiri kuwa CCM ni chama imara na kina mtaji mkubwa wa wanachama ambao mpaka sasa wanafikia Milioni 12 pamoja na wapenzi wengi, lakini alisisitza kuwa hiyo isiwe sababu ya kubweteka kwa mafanikio hayo na badala yeke wanatakiwa kupambana ili kuwatumikia Watanzania ili waione thamani ya chama kilichopewa ridhaa ya kuongoza Serikali yao.

"Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri" alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Vilevile katika hotuba yake Mwenyekiti huyo ametilia mkazo kuimarisha Jumuia ya vijana UVCCM, ambao ameitaja kuwa ndiyo itakayojenga chama imara kwa kuandaa viongozi wajao watakaokiendeleza chama hicho na baadaye kushika hatamu za uongozi.

Kuhusu Ajira kwa vijana Dkt Samia alisema, tayari wameanza kuboeresha Sekta ya Elimu wezeshi ambayo inatoa fursa kwa vijana kusomea mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri pamoja na kuajiri wenzao, pia masuala ya utalii, Uchumi wa Bluu pamoja na elimu ni miungoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima Mwezi Agisti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika Dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti Mzee Steven Wasira akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzaniua, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana




Inaendelea Uk. 13

# Dkt. Samia aja na mkakati kuondoa ukosefu wa ajira kwa vijana

Inatoka Uk. 12

madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.

Vilevile sherehe kama hizo zimefanyika maeneo mbalimbali ukiwemo mkoa wa Ruvuma ambapo

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa huo Oddo Mwisho alisema, uamuzi ya kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais wa Tanzania na Dkt Hussen Mwinyi kupeperusha Bendera ya Chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu ni sahihi kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya kwa Watanzania.

Mwisho, amewataka Wakazi wa Mkoa wa Ruvuma kutembea kifua mbele kutokana na maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

Aidha,amewasisitiza Wakazi wa Mkoa huo kutumia muda wao kujikita kwenye shughuli za uzalishaji mali hasa kilimo kwani Serikali imewekeza nguvu kubwa kwa kutoa pembejeo za ruzuku bure kwa Wakulima ili kuongeza uzalishaji na kuleta tija kwa Wakulima.

Katika hatua nyingne Mwisho,amewaagiza maafisa kilimo na maafisa Ushirika Mkoani Ruvuma, kuhakikisha wanatenda haki kwenye suala la ugawaji wa pembejeo kwa kuhakikisha kila mkulima ananufaika na matunda ya Serikali yake badala ya kugawa pembejeo hizo kwa upendeleo.

Pia,amewakumbusha Wanachama wa Chama hicho kutimiza wajibu wao kwa kueleza mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ili Wananchi wafahamu maendeleo yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka minne badala ya kukaa kimya.

Amewashukuru Wananchi wa Wilaya ya Tunduru kwa maamuzi sahihi kwa kuwachagua wagombea wa CCM kwenye Uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika mwaka uliopita ambapo Chama hicho kilipata ushindi ushindi wa kishindo.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Simon Chacha alisema,katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan wamepokea zaidi ya Sh.bilioni 300 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.



Kwa mujibu wa Chacha,fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi maji,elimu ,afya,umeme,Barabara,Mawasiliano,Utumishi na Utawala Bora na kuwezesha Wananchi wa Wilaya ya Tunduru kupata huduma bora za kijamii,kisiasa na Kiutamaduni.

Alisema,Sh.bilioni 5,598,853,033.85 zimetumika kujenga miundombinu ya vyumba vya madarasa,maabara za sayansi,m abweni, miundombinu ya vyoo na maji kwenye shule za Sekondari na Sh.bilioni 2,545,934,950.50 zimetumika kujenga miundombinu kama hiyo katika shule za msingi.



Katika sekta ya afya alisema,wamepokea Sh.bilioni 3,155,923,169.67 kujenga zahanati,vituo vya afya,nyumba za Watumishi, miundombinu ya vyoo na maji na Sh.bilioni 1,106,017,026.21 zimetumika kwenye mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mapato ya ndani(mikopo ya asilimia kumi).

Aidha, Halmashauri ya Wilaya imetumia Sh.bilioni 11,346,151,952 kuwezesha mpango wa kunusuru kaya maskini(Tasaf) , elimu bila malipo kwa shule za Sekondari,ujenzi wa miundombinu shule za msingi (BOOST) na pembejeo za kilimo.

Alisema,Wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini(Ruwasa) umepokea Sh.8,271,911,919.52, TARURA Sh.bilioni 10.500,Mamlaka ya maji Tunduru mjini Sh.bilioni 3.9, Tanesco Sh.bilioni 10.490,umeme vijijini (REA) Sh.bilioni 11.984 na miundombinu ya umeme Imara Sh.bilioni 245.980.

Naye Katibu Tawa la wa Wilaya ya Namtumbo Fransis Mgoloka alisema,katika kipindi cha miaka minne Wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh.bilioni 46.554 kati ya hizo Sh.bilioni 3.351 zimekwenda kwenye sekta ya afya,elimu Sh.bilioni 9, Sh.bilioni 8 umeme vijijini(REA) na sekta ya maji Sh.bilioni 7.8.

# YANGA YAMALIZA HASIRA KWA KEN GOLD

>> Inatoka uk. 16

Ramovic akiongea na Waandishi wa habari alisema kwamba ana kazi kubwa ya kuiongezea maarifa timu yake ili iweze kushinda kila mechi, iweze kutetea ubingwa wake lakini jioni yake mambo yakabadilika.

Wakati mashabiki wa Yanga wakiwa bado wanatafakari pigo hilo la kuodokewa na kocha wake ghafla habari zinabainisha kuwa aliyekuwa kocha wa Singida Black Stars, Hamdi Miloud Raia wa Algeria aliwasili Jijini fasta akitokea Singida tayatri kutwaa mikoba ya mtangulizi wake huyo, kuwatumikia wananchi.

Kocha huyo alitua akiwa na msaidizi wake tayari kuanza majukumu mapya ndani ya klabu ya Yanga na jana alionekana jukwaani akikishuhudia kikosi chake kipya kikitoa adhabu dhidi ya Ken Gold.

Tayari Yanga imeshamtangaza kocha huyo mwenye uraia wa Algeria na Ufaransa kuwa kocha wake mpya akichukua mikoba ya Sead Ramovic ambaye aliyeomndoka klabuni hapo baada ya kuvunja naye mkataba kwa makubaliano ya pande zote mbili.



# VAR YAZAA MATUNDA UWANJANI

>> Inatoka uk. 16

za wachezaji ."

Katika kesi ya Erik ten Hag, hilo ndilo lililotokea - moja ya makosa manne ilikuwa adhabu iliyotolewa dhidi ya timu yake ya Manchester United katika mechi ambayo ilionekana kuwa mechi yake ya mwisho.

Waamuzi pia wamekuwa wakidhulumiwa, huku polisi hivi majuzi wakichunguza "vitisho na unyanyasaji" uliyoelekezwa kwa Michael Oliver kufuatia ushindi wa Arsenal wa 1-0 dhidi ya Wolves mnamo Januari.

Oliver kwa utata alimtoa kwa kadi nyekundu beki wa Gunners Myles Lewis-Skelly - uamuzi ambao ulibatilishwa baada ya kukata rufaa.

Aliyekuwa mwamuzi David Coote alifutwa kazi na bodi ya waamuzi mwezi Disemba baada ya "uchunguzi wa kina" kuhusu mwenendo wake.

Alipoulizwa kuhusu imani kwa viongozi, Scholes alisema: "Sote tuna jukumu la kuwa na usawa katika maoni ambayo yanatolewa.

"Hatuwezi kuwa na viongozi, sehemu muhimu ya ligi yenye mafanikio na burudani, inayokabiliwa na aina ya unyanyasaji unaotokea mara kwa mara.

"Watu hawa ni wazuri. Najua huo sio mtazamo kila wakati, lakini ulimwengu wote unatambua jinsi walivyo wazuri."


Ligi ya Premia ilikataa kuorodhesha hatua tisa zenye makosa - na iwapo hatua hizo ni pamoja na kadi nyekundu ya Lewis-Skelly. Ilielezea makosa manne kwa vyombo vya habari.

# RASHFORD ATUA ASTONVILA

BARCELONA, HISPANIA

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford wamekutana na viongozi wa Antonvila siku ya Jumanne huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitafuta njia ya kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Rashford kumekuwa na uvumi wa kutakiwa na timu kadhaa, hivyo kuzidi kufanya uvumi wa kuondoka kwake kushika kasi zaidi, huku hayo yakija wakati Paul Scholes akisema, ndani ya kikosi hicho kuna wachezaji wanane wabovu.




# LUIZ ANAKWENDA HAPA

MILAN, IITALIA

TIMU ya Juventus wameipa Chelsea fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal.

Hayo yaja huku kiungo wa Ufaransa Paul Pogba, 31, anazingatia ofa kadhaa kutoka kwa timu za ligi tano kuu za Ulaya, lakini makubaliano ya mkataba hayajafikiwa.



# P-SQUARE
## ‘Mapacha’ ndani ya mgogoro!-3

LOGOS, NIGERIA

NI lazima nieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, “aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. “Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza.”

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. “Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha.”

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia ‘mixtape’ yake ya ‘Room for Improvement.’

# Tamasha la muziki ‘Kadanse ya Mama’ yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.

Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.


Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz ‘Wanamsondo ngoma’ ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.





UK.15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA
# MICHEZO

ALHAMISI Februari 06, 2025 Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

# Yanga yamaliza hasira kwa Ken Gold

## >> Yaichakaza mabao 6-1 bila huruma



NA MWANDISHI WETU

MABINWA watetezi Yanga ya Dar es Salaam jana iliendeleza ubabe katika michuano ya Ligi Kuu ya NBC, baada ya kuifunga mabao 6-1, huku alaiyekuwa Kocha wake Mkuu Sead Ramovic akijindoa kuifundidsha klabu hiyo na kutimkia nchini Morocco.

Taarifa zilizotolewa na Klabu hiyo kongwe nchini inasema kuwa, kocha huyo alivunja mkataba ghafla katika Klabu hiyo ya Wananchi, huku ikidaiwa anakwenda nchini Morocco alikopata kibarua cha kuinoa klabu ya CR Belouizdad iliyomtengea donge nono.

Juzi asubuhi Kocha

Inaendelea Uk.14

# VAR YAZAA MATUNDA UWANJANI

NA MWANDISHI WETU

KUMEKUWA na makosa 13 ya waamuzi wasaidizi wa video (VAR) katika Ligi ya Premia hadi sasa msimu huu yakiwa ya chini kutoka 20 yaliofanyika katika hatua kama hiyo muhula uliopita.

Hatua nne zisizo sahihi za VAR na uingiliaji kati mara tisa uliofanyika kimakosa kutoka kwa mzunguko wa mechi za kwanza 23 zimegunduliwa na jopo la Matukio Muhimu ya Mashindano (KMI).


Kumekuwa na uingiliaji kati mara 70 wa VAR katika mechi 239 za ligi msimu huu - karibu moja katika kila mechi tatu.

Ligi hiyo inasema usahihi wa 'Matukio Muhimu ya Mechi' ni 96.4% - kutoka 95.7% katika hatua inayolingana muhula uliopita.

"Hakuna mtu anayedharau umuhimu na athari ya kosa moja," afisa mkuu wa kandanda Tony Scholes alisema.

"Tunajua kwamba kosa moja linaweza kugharimu klabu. Pointi na matokeo yanaweza kuathiri nafasi za wasimamizi, na nafasi

Inaendelea Uk.14



# Unaikumbuka Marijani na Vick?

NA MWANDISHI WETU

WAKATI ikikaribia kumbukuzi la kifoi cha mwanamuziki mahiri aliyewahi kuokea katika ardhi ya bTanzania Marijan Rajab, leo tukumbuke moja ya nyimbo zlizotunga enzi ya uhai wake.

Marijani alianza kutamba katika tasnia ya muziki akiwa na bendi ya STC mwaka 1970 hadi 71, kisha akahamia katika bendi ya Safari Trippers mwaka 1972 na kurekodi albam ya kwanza tarehe 19.1.1972,



yenye nyimbo kama Rosa nenda Shule, Mkuki Moyoni, Rafiki si mtu mwema na nyingine kadha.

"VICK ee ungenijulisha mapema, mawazo kama yamebadilika ili niweze kumtafuta mwingine awezaye kulisakata "Bomboka", usinikondeshe buree mwana wa mwenzio, wakati wewe mwenyewe hata hunijali, hebu nijulishe Vick ee ili nijue moja"...

Haya ni maneno

Inaendelea Uk.15

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM